Washington State Health Care Authority

Washington State Department of Social & Health Services — Transforming lives

# Haki na Wajibu wa Bima ya Afya

Health Care Coverage Rights and Responsibilities

## Haki Zako (tunapaswa) kwa programu zote za bima ya afya

**Kukusaidia kusoma na kujaza fomu zote zinazohitajika.** Unaweza kuwasiliana na Idara ya Huduma za Afya na Jamii (DSHS) kupitia 1-877-501-2233 kwa usaidizi.

**Kukupatia huduma za ukalimani na utafsiri** bila gharama yoyote na bila kuchelewa wakati unapowasiliana na DSHS au Mamlaka ya Huduma ya Afya (HCA).

**Kutunza faragha ya taarifa zako binafsi** ila tunaweza kushirikisha baadhi ya taarifa kwa mashirika mengine ya jimbo na serikali kuu, taasisi za kifedha, na wakandarasi wa HCA kwa madhumuni ya ustahiki na uandikishaji.

**Kukupa fursa ya kukata rufani** usipokubaliana na ubainifu uliofanywa na DSHS au HCA ambao unaathiri ustahiki wako wa kinga ya afya, huduma na usaidizi wa muda mrefu (LTSS), au bima ya afya. Ukiomba kukata rufani, kesi yako itafanyiwa mapitio. Kwa taarifa kuhusu kukata rufani za programu za DSHS, wasiliana na Kituo cha Huduma kwa Wateja cha DSHS kupitia 1-877-501-2233 au tembelea Ofisi ya Huduma kwa Jumuiya.

Ikiwa rufani inakatwa kwa uamuzi wa bima ya Washington Apple Health, ambao haujatatuliwa kwa mapitio ya kesi, utapangiwa Usikilizaji wa Shauri la Kiutawala.

**Kukutendea kwa haki. Ubaguzi ni kinyume cha sheria.** DSHS na HCA zinatii sheria zinazohusika na haki za kiraia za Serikali Kuu na hazifanyi ubaguzi kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu, au jinsia. DSHS na HCA haziwatengi watu au kuwatendea tofauti kwa sababu ya mbari, rangi, asili ya utaifa, umri, ulemavu, au jinsia yao.

DSHS na HCA pia zinatii sheria husika za jimbo na hazibagui kwa misingi ya imani, udhihirisho au utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kingono, hali ya ndoa, dini, mwanajeshi aliyestaafu kwa heshima au hali ya kijeshi, au utumiaji wa mbwa mwongozi aliyepewa mafunzo au mnyama ambaye anamhudumia mtu mwenye ulemavu.

DSHS na HCA:

- Zinatoa usaidizi bila malipo na huduma kwa watu wenye ulemavu ili waweze kuwasiliana nasi kwa ufanisi, kama vile:
  - Wakalimani wa lugha ya ishara wenye sifa
  - Taarifa ya maandishi kwa muundo mwingine (herufi kubwa, sauti, miundo ya kielekroniki kwa walemavu, mifumo mingine)
- Wanatoa huduma za lugha bila malipo kwa watu ambao lugha yao ya kwanza si Kiingereza, kama vile:
  - Wakalimani wenye sifa
  - Taarifa iliyoandikwa kwa lugha nyingine

Ikiwa unahitaji huduma hizi, piga namba 1-877-501-2233.

Ukiamini kwamba DSHS au HCA zimeshindwa kutoa huduma hizi au umebaguliwa kwa namna nyingine, unaweza kuwasilisha lalamiko katika:

- **DSHS**
  ATTN: Constituent Services
  PO Box 45131
  Olympia, WA 98504-5131
  1-800-737-0617
  Faksi: 1-888-338-7410
  **askdshs@dshs.wa.gov**
- **HCA Division of Legal Services**
  ATTN: Compliance Officer
  PO Box 42704
  Olympia, WA 98504-2704
  1-855-682-0787
  Faksi: 1-360-586-9551
  **compliance@hca.wa.gov**

Unaweza kuwasilisha lalamiko wewe mwenyewe au kwa simu, barua, faksi, au barua pepe. Ukihitaji msaada kuwasilisha lalamiko, Huduma za Jimbo za DSHS au Divisheni ya Huduma za Kisheria ya HCA zinapatikana ili kukusaidia.

Unaweza pia kufungua lalamiko la haki za kiraia kielektroniki katika Idara ya Huduma za Binadamu na Afya ya Marekani, Ofisi ya Haki za Kiraia kupitia **https://ocrportal.hhs.gov/ocr/portal/lobby.jsf,** au kwa barua au simu kupitia:

**U.S. Department of Health and Human Services**
200 Independence Avenue SW
Room 509F, HHH Building
Washington, D.C. 20201
1-800-368-1019, 800-537-7697 (TDD).

Fomu za malalamiko zinapatikana kupitia **www.hhs.gov/ocr/office/file/index.html.**

## Majukumu Yako (unapaswa) kwa programu zote za bima ya afya

**Kufichua SSN na Hali ya Uhamiaji.** Isipokuwa kwa baadhi ya watu, unapaswa kutoa Nambari ya 'Social Security' (SSN) au nambari ya hati ya uhamiaji ya kwako au yeyote katika kaya yako anayetaka kuomba bima ya afya. SSN inahitajika ili kuomba fedha za kodi (tax credits) za ada za bima ya afya. Tunatumia taarifa hii kubaini ustahiki wako kwa kuthibitisha utambulisho wako, uraia wako, hali yako ya uhamiaji, tarehe ya kuzaliwa, na upatikanaji wa bima nyingine za afya. Hatushirikishi taarifa zako hizi kwa shirika lolote la uhamiaji.

Inawezekana kuomba bima kwa baadhi ya watu wa kaya yako, lakini si wengine. Ikiwa huna SSN au nambari ya hati ya uhamiaji kwa watu wote wa kaya, wengine bado wanaweza kuomba na kupata bima. Kwa mfano, unaweza kuomba kwa ajili ya mtoto wako ikiwa wewe huna ustahiki wa bima. Kuomba bima hakuwezi kuathiri hali yako ya uhamiaji au uwezekano wa kuwa mkazi wa kudumu au raia.

Pia kuna baadhi ya programu za Washington Apple Health kwa watu wasioweza kuthibitisha kuwa wapo nchini kihalali. Lakini ukiamua kutotoa SSN au nambari ya hati ya uhamiaji ya mtu mwingine katika kaya yako, tutahitaji kufanya ufuatiliaji kwako ili kupata taarifa kuhusu kipato cha mtu asiyeomba bima.
**Ikiombwa na shirika,** toa taarifa yoyote au ushahidi ambao unahitajika kuamua kama una ustahiki.

## Mambo unayotakiwa kuyajua kwa programu zote za bima ya afya

**Kuna baadhi ya sheria za jimbo na za serikali kuu** ambazo zinasimamia utendaji wa Washington Connection na mifumo ya maombi inayoedneshwa na jimbo, haki na wajibu wako kama mtu anayeitumia mifumo hiyo na kinga ya bima ambayo unaipata kwa kuitumia mifumo hiyo. Kwa kutumia mifumo hii, unakubali kutii sheria zinazohusika kwa mtu anayetumia mifumo hiyo na kinga ya bima anayopata kutokana na kutumia mifumo hiyo.

**Sheria ya Taifa ya Usajili wa Mpiga Kura ya 1973** inahitaji majimbo yote kutoa usaidizi wa usajili wa mpiga kura kupitia ofisi zao za msaada kwa umma. Kuomba kujiandikisha au kukataa kujiandikisha kupiga kura hakutaathiri huduma au mafao ambayo utapatiwa na shirika hili. Jiandikishe kupiga kura hapa **www.vote.wa.gov** au omba fomu za kuandikisha mpiga kura 1-800-448-4881.

**Vikwazo vya Sheria ya Uhamishaji na Uwajibikaji wa Bima ya Afya (HIPAA)** vinaizuia HCA na DSHS kujadili taarifa ya kiafya ya kwako au mtu yeyote wa kaya yako na mtu yeyote, ikiwemo mwakilishi aliyeidhinishwa, isipokuwa tu kama mtu huyo awe na mamlaka ya uwakilishi (power of attorney) au iwapo wewe umesaini fomu ya ridhaa ukiidhinisha ufichuzi wa taarifa hii. Hii inajumuisha ufichuzi wa taarifa ya afya ya akili, VVU, UKIMWI, majibu ya vipimo vya Magonjwa ya Zinaa, au matibabu na huduma za utegemezi wa kemikali.

**Sheria ya Matibabu Nafuu** inaizuia DSHS na HCA kutoa taarifa zenye utambulisho binafsi (PII) za kwako au mtu yeyote wa kaya yako kwa mtu yeyote ambaye hajaidhinishwa kuzipokea, na bila ridhaa yako.

**Taarifa ambayo unaipa DSHS na HCA** itafanyiwa uthibitisho na maafisa wa serikali kuu na wa jimbo kwa madhumuni ya kubaini ustahiki wako wa kinga ya bima ya afya. Uthibitishaji unaweza kujumuisha kuendesha ufuatiliaji wa wahusika utakaofanywa na wafanyakazi wa shirika.

**HCA na DSHS haziwajibiki kwa usimamiaji wa bima yako ya afya.** Kampuni yako ya bima ya afya inaweza kukupa taarifa zaidi kuhusu mafao yako. **Ukiwa na maswali kuhusu vigezo vya bima yako ya afya, ikiwemo mafao yapi una ustahiki nayo, na kudai mafao au kukata rufani ya kukataliwa mafao, unapaswa kuwasiliana na kampuni yako ya bima ya afya.**

**Unaweza kuomba huduma za kushurutisha matunzo kupitia Divisheni ya Matunzo ya Watoto (DCS).** Kupata maombi ya huduma hizi, tembelea **www.childsupportonline.wa.gov** au wasiliana na ofisi yako mahalia ya DCS.

## Haki Zako (tunapaswa) kwa bima ya Washington Apple Health tu

**Kukuelezea haki na wajibu wako** ikiwa utaomba hivyo.

**Kukuruhusu kutuma sehemu ya maombi** inayojumuisha angalau, jina lako, anwani, saini yako au saini ya mwakilishi aliyeidhinishwa wa mwombaji. Siku tunayopata sehemu ya maombi ndyo tarehe ya maombi yako, ambayo inaweza kuathiri lini bima yako itatmika rasmi. Hatutatoa uamuzi wa mwisho kuhusu bima yako hadi baada ya kuwa umekamilisha maombi yako.

**Kukuruhusu kuwasilisha maombi au sehemu ya maombi yako** kwa kutumia njia iliyoainishwa chini ya WAC 182-503-0005.

**Kushughulikia maombi yako haraka** na sio zaidi ya muda ulioainishwa katika WAC 182-503-0060.

**Kukupa siku 10 za kalenda** kutupatia taarifa tunazohitaji ili kubaini ustahiki. Ukiomba muda zaidi, tutakupa muda zaidi. Usipotupatia taarifa au usipoomba muda zaidi, tunaweza kukunyima, kuifunga, au kuibadili bima yako ya afya.

**Kukusaidia** ukipata changamoto kupata taarifa yoyote au ushahidi unaohitajika kwetu ili kuamua kama una ustahiki. Kama tutahitaji nyaraka ambayo inagharimu fedha, tutaiomba na tutalipa gharama.

**Kukutaarifu, kadri iwezekanavyo, angalau siku 10** kabla ya kusitisha kinga ya bima yako ya afya.

**Kukupa maamuzi ya maandishi,** kwenye kesi nyingi, ndani ya siku 45. Kinga ya Bima ya afya kwa baadhi ya kesi za ulemavu inaweza kuchukua hadi siku 60. Tunatoa uamuzi wa maandishi kwa matibabu ya ujauzito ndani ya siku 15.

**Kukuruhusu kukataa kuzungumza** na mchunguzi ikiwa tunafanya ukaguzi wa kesi yako. Hulazimiki kumruhusu mchunguzi aingie nyumbani kwako. Unaweza kumwomba mchunguzi aje wakati mwingine. Ombi kama hilo halitaathiri ustahiki wako wa kinga ya bima ya afya.

**Kuendelea na kinga ya bima ya Washington Apple Health** wakati tukiamua iwapo una ustahiki wa programu nyingine kwa mujibu wa WAC 182-504-0125.

**Kukupa huduma za haki sawa za ufikio** kama ilivyoelezewa katika WAC 182-503-0120 ikiwa una ustahiki.

## Wajibu wako (unapaswa) kwa Washington Apple Health tu

**Kuripoti mabadiliko kama inavyotakiwa** katika WAC 182-504-0105 na WAC 182-504-0110 ndani ya siku 30 za badiliko. Kusoma barua yako ya idhinisho ili kuona ni mabadiliko gani unapaswa kuyaripoti.

**Kufufua bima** ukiombwa kufanya hivyo.

**Kutoa taarifa za watoa huduma ya kitiba** inayohitajika kututoza sisi kwa ajili ya huduma za afya.

**Kuomba Medicare** ikiwa una haki ya kuwa nayo.

**Kutoa ushirikiano kwa watu wa Uhakikisho wa Ubora** pale inapohitajika.

**Kuomba na kufanya jitihada ya kutosha** kupata kipato kutoka vyanzo vingine wakati unaomba au kupokea kinga ya bima ya Washington Apple Health.

## Mambo unayotakiwa kuyajua kwa bima ya Washington Apple Health tu

**Kwa kuomba na kupokea Washington Apple Health,** unalipa jimbo la Washington haki zote za usaidizi wowote wa kitiba na za malipo ya wahusika wa tatu wa huduma ya afya.

**Shirika linaweza kutoa** historia ya chanjo ya mtoto wako kwa Mfumo wa Kufuatilia Chanjo za Watoto (CPITS).

**Taarifa unayoripoti** inaweza kushirikishwa kwa DSHS ili kubaini ustahiki na mafao ya kila mwezi kwa programu kama vile kinga ya bima ya afya, usaidizi wa pesa taslimu, usaidizi wa chakula na ruzuku za ulezi wa watoto.

**Kisheria, Jimbo la Washington linaweza kurejesha gharama ilizolipa kwa huduma za aina fulani za kitiba kutoka kwenye mali yako ya urithi kupitia 'Estate Recovery' (RCW 41.05A.090, RCW 43.20B.080, na Chapter 182-527 WAC).** 'Estate Recovery' haifanyiki hadi baada ya kifo chako, kifo cha mwenzi wako aliyesalia, na watoto wako waliosalia wawe na miaka 21 au zaidi. Pia haifanyiki ikiwa mtoto aliyesalia alikuwa kipofu/mlemavu wakati wa kifo chako. Gharama zinazopaswa kurejeshwa zinajumuisha:

- Baadhi ya huduma na usaidizi wa muda mrefu wa Washington Apple Health, ikiwa ulikuwa na miaka 55 au zaidi wakati ulipopokea huduma;
- Baadhi ya huduma zinazofadhiliwa na jimbo tu, bila kujali umri wako wakati ulipopokea huduma.

Unaweza kupata orodha ya huduma zinazopaswa kurejeshwa gharama kwenye WAC 182-527-2742. Unaweza kupata orodha ya mali zisizohusika katika urejeshaji kwa mujibu wa WAC 182-527-2746.

Jimbo linaweza pia kufaili umiliki kabla ya kifo wa nyumba yako, katika umri wowote, ikiwa utawekwa kwenye taasisi kwa kipindi cha maisha yako yote (WAC 182-527-2734). Jimbo linaweza kurejesha gharama baada ya mauzo ya nyumba, au mali yako ya urithi, isipokuwa:

- Mwenzi wako anaishi katika nyumba hiyo;
- Ndugu yako anaishi katika nyumba hiyo, ni mmiliki mwenza, na anakidhi baadhi ya vigezo;
- Mtoto wako anaishi katika nymba hiyo, na ni kipofu/mlemavu; au
- Mtoto wako anaishi katika nyumba hiyo na ana chini ya miaka 21.

Pata orodha ya huduma zinazopaswa kurejeshwa gharama chini ya umiliki kabla ya kifo katika WAC 182-527-2734.

**Unaweza kuwekewa ukomo wa mtoa huduma mmoja,** duka moja la dawa, na/au hospitali moja ikiwa utaomba huduma za afya zisizo za lazima kutoka kwa watoa huduma.

Washington State
Health Care Authority

[English] Language assistance services, including interpreters and translation of printed materials, are available free of charge. Call 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Amharic] የቋንቋ እገዛ አገልግሎት፣ አስተርጓሚ እና የሰነዶችን ትርጉም ጨምሮ በነጻ ይገኛል፡፡ 1-800-562-3022 (TRS: 711) ይደውሉ፡፡

[Arabic] خدمات المساعدة في اللغات، بما في ذلك المترجمين الفوريين وترجمة المواد المطبوعة، متوفرة مجاناً، اتصل على رقم 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Burmese] ဘာသာပြန်ဆိုသူများနှင့် ထုတ်ပြန်ထားသည့် စာရွက်စာတမ်းများဘာသာပြန်ခြင်းအပါအဝင် ဘာသာစကားအထောက်အကူဝန်ဆောင်မှုများကို အခမဲ့ရနိုင်ပါသည်။ 1-800-562-3022 (TRS: 711) ကိုဖုန်းခေါ်ဆိုပါ။

[Cambodian] សេវាជំនួយភាសា រួមមានទាំងអ្នកបកប្រែផ្ទាល់មាត់ និង ការបកប្រែឯកសារបោះពុម្ព គឺអាចរកបានដោយឥតគិតថ្លៃ។ ហៅទូរស័ព្ទទៅលេខ 1-800-562-3022 (TRS: 711)។

[Chinese] 免费提供语言协助服务，包括口译员和印制资料翻译。请致电 1-800-562-3022 (TRS: 711)。

[Farsi (Persian)] خدمات کمک زبانی، از جمله مترجم شفاهی و ترجمه اسناد و مدارک (مطالب) چاپی، بصورت رایگان ارائه خواهد شد.با شماره 1-800-562-3022 (TRS: 711) تماس بگیرید.

[French] Des services d’aide linguistique, dont des interprètes et la traduction des documents, sont disponibles gratuitement. Appelez le 1-800-562-3022 (TRS : 711).

[Korean] 통역 서비스와 인쇄 자료 번역을 포함한 언어 지원 서비스를 무료로 이용하실 수 있습니다. 1-800-562-3022 (TRS: 711)번으로 전화하십시오.

[Laotian] ການບໍລິການດ້ານພາສາ, ລວມທັງນາຍແປພາສາ ແລະ ການແປເອກະສານທີ່ພິມ, ມີໄວ້ໃຫ້ຟຣີໂດຍບໍ່ຄິດຄ່າ. ໂທຫາເລກ 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Pashto] په انګلیسي ژبه باندې دپوهیدلو، په شمول د ژباړونکي او د چاپ شوي موادو ژباړه کولو د مرستې خدمتونه، پرته له تادیې په وړیا توګه شتون لري. دې خدمت ته لاسرسي موندلو لپاره دې شمېرې 1-800-562-3022 ته زنګ ووهئ (د اوریدلو یا خبرو کولو معلولیت لرونکې خلکو د زنګ وهلو شمېره (TRS): 711)

[Portuguese] Serviços de assistência linguística, incluindo interpretação e tradução de versões impressas, estão disponíveis gratuitamente. Ligue para 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Punjabi] ਭਾਸ਼ਾ ਸਹਾਇਤਾ ਸੇਵਾਵਾਂ—ਦੁਭਾਸ਼ੀਏ ਅਤੇ ਪ੍ਰਿੰਟ ਕੀਤੀ ਹੋਈ ਸਮੱਗਰੀ ਦੇ ਅੰਨੁਵਾਦ ਸਮੇਤ—ਮੁਫ਼ਤ ਉਪਲੱਬਧ ਹਨ। 1-800-562-3022 (TRS: 711) 'ਤੇ ਕਾਲ ਕਰੋ।

[Russian] Языковая поддержка, в том числе услуги переводчиков и перевод печатных материалов, доступна бесплатно. Позвоните по номеру 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Somali] Adeego caawimaad luuqada ah, ay ku jirto turjubaano afka ah iyo turjumid lagu sameeyo waraaqaha la daabaco, ayaa lagu helayaa lacag la’aan. Wac 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Spanish] Hay servicios de asistencia con idiomas, incluyendo intérpretes y traducción de materiales impresos, disponibles sin costo. Llame al 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Tagalog] Mga serbisyong tulong sa wika, kabilang ang mga tagapagsalin at pagsasalin ng nakalimbag na mga kagamitan, ay magagamit ng walang bayad. Tumawag sa 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Tigrigna] ተርጎምትን ናይ ዝተፅሓፉ ማተርያላት ትርጉምን ሓዊሱ ናይ ቋንቋ ሓገዝ ግልጋሎት፤ ብዘይ ምንም ክፍሊት ይርከቡ፡፡ ብ 1-800-562-3022 (TRS: 711) ደውሉ፡፡

[Ukrainian] Мовна підтримка, у тому числі послуги перекладачів та переклад друкованих матеріалів, доступна безкоштовно. Зателефонуйте за номером 1-800-562-3022 (TRS: 711).

[Vietnamese] Các dịch vụ trợ giúp ngôn ngữ, bao gồm thông dịch viên và bản dịch tài liệu in, hiện có miễn phí. Gọi 1-800-562-3022 (TRS: 711).